"Nyofoo"

# HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA UKUMBI WA MIKUTANO TAREHE 03/11/2021

### A. WAJUMBE WALIOHUDHURIA

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mh. Yusto M. Mapande | - | Diwani Kata ya Msindo | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mh. Mhina E. Mmasa | - | Diwani Kata ya Bendera | - | Makamu M/Kiti |
| 3. | Mh. Habiba R. Irigo | - | Diwani V/ Maalum Hedaru | - | Mjumbe |
| 4. | Mh. Mariane A. Mariane | - | Diwani Kata ya Kihurio | - | Mjumbe |
| 5. | Mh. Elisa D. Mnguruta | - | Diwani Kata ya Mtii | - | Mjumbe |
| 6. | Mh. Nzota T. Koishwa | - | Diwani Kata ya Luguli | - | Mjumbe |
| 7. | Mh. Grace G. Kiangi | - | Diwani V/ Maalum Myamba | - | Mjumbe |
| 8. | Mh. Heriel E. Mjema | - | Diwani Kata ya Stesheni | - | Mjumbe |
| 9. | Mh. Jamila s. Mdee | - | Diwani V/ Maalum Mwembe | - | Mjumbe |
| 10. | Mh. John R. Msofe | - | Diwani Kata ya Vumari | - | Mjumbe |

### B. WAJUMBE WASIOHUDHURIA

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mh. David Mathayo | - | Mbunge Same Magharibi | - | Kwa Taarifa |
| 2. | Mh. Anne Kilango | - | Mbunge Same Mashariki | - | Kwa Taarifa |

### C. WATENDAJI WALIOHUDHURIA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Anastazia Tutuba | - | Mkurugenzi Mtendaji (W) - Katibu |
| 2. | Ndg. Rogath G. Nlula | - | Mkuu wa Idara ya Utumishi (W) |
| 3. | Ndg. Meshack J. Kingu | - | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (W) |
| 4. | Ndg. Anjela R. Mnjokava | - | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA (W) |
| 5. | Ndg. Charles Anatoly | - | Kaimu Mkuu wa Idara Maendeleo ya Jamii (W) |
| 6. | Ndg. Uledi Lusasi | - | Mtendaji Mkuu Mamlaka ya Mji Mdogo Same |
| 7. | Ndg. Upendo Kivuyo | - | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria (W) |
| 8. | Ndg. Ally Mngwaya | - | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili (W) |
| 9. | Dr. Cainan Kiswaga | - | Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi (W) |
| 10. | Ndg. Genge M. Charles | - | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara (W) |
| 11. | Ndg. Omary Mhina | - | Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W) |
| 12. | Ndg. Prisca P. Sima | - | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Nyuki (W) |
| 13. | Ndg. Marunda Michael | - | Mratibu wa Viashiria Hatarishi (W) |
| 14. | Ndg. Swai M. Aidan | - | Afisa Biashara (W) |
| 15. | Ndg. Nzinyangwa Mchomvu | - | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi (W) |
| 16. | Ndg. Hamadi Mfinanga | - | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi (W) |
| 17. | Ndg. Victoria Komba | - | Mratibu wa UKIMWI |
| 18. | Ndg. Iddi Goa | - | Mhasibu wa Mapato |
| 19. | Ndg. Amri Samsoni | - | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi (W) |
| 20. | Ndg. Helen Mshana | - | Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi (W) |
| 21. | Ndg. Addinani Mwenda | - | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari (W) |

22. Ndg. Angelina K. Sampa - Afisa Ardhi Mteule
23. Ndg. Mary A. Kanumba - Mkuu wa Idara ya Mipango (W)
24. Ndg. Tumaini J. Lyatuu - Mratibu wa TASAF (W)
25. Ndg. Fabian Bulili - Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya (W)
26. Ndg. Kitwana Mungi - Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira (W)

**D. SEKRETARIETI**

1. Ndg. Ester E. Mchome
2. Ndg. Simon G. Maeda

**AGENDA NA. 01:- KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alianza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa ulinzi hadi siku ya kikao. Alieleza kuwa kikao hicho ni cha kawaida, aliwapa pongezi wajumbe kwa ziara iliyofanyika. Baada ya maelezo hayo akidi ilikuwa imetimia ndipo alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao.

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe alisema kuwa ni kikao cha kawaida cha Kamati. Aliwahimiza wajumbe kuchangia katika agenda zilizoandaliwa kisha alifungua kikao saa 05:47 asubuhi.

**AGENDA NA. 15:- TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

Afisa Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji (W) aliwasilisha taarifa ya mapokezi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo alieleza kuwa Halmashauri kwa kipindi cha mwezi Septemba – Oktoba imepokea jumla Tshs. 2,058,852,352.51 fedha za ruzuku zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta za Afya na Elimu.

Fedha hizi zimetolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia mpango wa lipa kwa matokeo (EP4R), Fedha za mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVICO19 fedha za ujenzi wa vituo vya afya katika tarafa ya Gonja pamoja na fedha za ujenzi wa madarasa ya Sekondari kwa fedha za Serikali kuu.

Mchanganuo wa kiasi cha fedha na miundombinu itakayotekelezwa ni kama ifuatavyo;

| JINA LA MRADI | CHANZO CHA FEDHA | KIASI KILICHOTOLEWA |
|---|---|---|
| Ujenzi wa madarasa 56 katika Shule za Sekondari | GAVI | 1,120,000,000.00 |
| Ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum shule ya msingi Same | GAVI | 80,000,000.00 |
| Umaliziaji wa madarasa 4, madarasa 3 Vunta na Kirangare 1 | Serikali Kuu | 50,000,000.00 |
| Ujenzi wa mifumo ya kunawia mikono, uvunaji wa maji, uwekaji wa maji ya bomba, uchimbaji wa visima virefu Shule za Msingi Kishaa, Jiungeni na Sekondari ya Ndungu | GAVI/IMF | 35,617,139.58 |

| | | |
|---|---|---|
| Ujenzi wa matundu ya vyoo katika Shule za Msingi za Chanika na Jiungeni | EP4R | 13,200,000.00 |
| Fedha za uendeshaji wa zoezi la chanjo ya UVICO19 | GAVI/IMF | 35,035,212.93 |
| Ujenzi wa kituo cha afya Tarafa Za Gonja na Same | Serikali kuu | 500,000,000.00 |
| Ujenzi wa madarasa ya shule za Sekondari | Serikali kuu | 225,000,000.00 |
| Jumla kuu | | 2,058,852,352.51 |

Wajumbe walijadili na kuridhia taarifa hiyo.

**AGENDA NA. 18:- ONGEZEKO LA MPANGO WA MANUNUZI WA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KUTOKA TSHS. 5,029,960,012.92 HADI TSHS. 6,828,777,152.00**

Kaimu Afisa Manunuzi (W) aliwasilisha taarifa ya ongezeko la mpango wa manunuzi wa mwaka wa fedha 2021/2022 kutoka Tshs. 5,029,960,012.92 hadi Tshs. 6,828,777,152.00 ambapo alieleza kuwa ni kutokana na kupata fedha za miradi ya afya na elimu yenye jumla ya Tshs. 1,798,817,140.00 na mchanganuo wake ni kama ifuatavyo;-

| JINA LA MRADI | CHANZO CHA FEDHA | KIASI KILICHOTOLEWA |
|---|---|---|
| Ujenzi wa madarasa 56 katika Shule za Sekondari. | Gavi | 1,120,000,000/= |
| Ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum | Gavi | 80,000,000.00 |
| Umaliziaji wa madarasa 4 madarasa 3 Vunta na Kirangare 1 | Serikali kuu | 50,000,000.00 |
| Ujenzi wa vituo vya afya na tarafa | Serikali kuu | 500,000,000.00 |
| Ujenzi wa mifumo ya kunawia mikono, uvunaji wa maji, uwekaji wa maji ya bomba, uchimbaji wa visima Shule za Msingi Kishaa, Jiungeni na Sekondari Ndungu | Gavi | 35,617,139.58 |
| Ujenzi wa matundu ya vyoo katika Shule za Msingi za Chanika na Jiungeni. | EP4R | 13,200,000.00 |
| Jumla kuu | | 1,798,817,140.00 |

Wajumbe walipokea, kujadili na kuridhia taarifa hiyo.

| | | |
|---|---|---|
| | | eneo hilo ili kusiwe na ujenzi wa holela.<br>- Barabara ambayo inatumika kwenye eneo la ujenzi wa hospitali TARURA waombwe ili iingizwe kwenye mtandao wa barabara za Wilaya<br>- Iandikwe barua ya kuishukuru Serikali ya Kijiji cha Nasuro kwa kutoa eneo la ujenzi wa Hospitali ya Wilaya pamoja na soko la barabarani.. |

Wajumbe walijadili na kuridhia taarifa hiyo.

**AGENDA NA. 19:- KUFUNGA KIKAO**
Mwenyekiti alifunga kikao saa 9:30 jioni.

## U M E T H I B I T I T I S H W A

| ................................ | 03/12/2021 | ................................ | 03.12.2021 |
|---|---|---|---|
| **KATIBU** | **TAREHE** | **MWENYEKITI** | **TAREHE** |